JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# UTAFITI WA WATU WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI TANZANIA (ILFS) - 2014

## MWONGOZO WA KUDHIBITI UBORA

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU
WIZARA YA FEDHA
DAR ES SALAAM

**MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KUKAGUA KAZI YA UTAFITI WA MAJARIBIO WA WATU WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI WA MWAKA 2014 - (QUICK CHECKS)**

Kama tulivyokubaliana wakati wa mafunzo, kutokana na matakwa makubwa ya Nchi, ILO, EAC, SADC na AU, kuna mabadiliko makubwa kwenye dodoso la 2014 ILFS ikilinganishwa na lile la mwaka 2006. Hivyo tunaomba Msimamizi awe makini sana wakati wa kukagua kazi kwa kuzingatia mambo yafuatayo ili tuweze kupata viashiria vinavyokusudiwa na vyenye kiwango kinachotakiwa;

## 1) MAMBO YA KUZINGATIA KWA UJUMLA

Kila Msimamizi anatakiwa ahakikishe amekagua kazi nzima kwa umakini kabisa kabla madodoso hayajarudishwa Makao Makuu. Kama kuna makosa ambayo yanahitaji kurudi kwenye kaya inabidi ifanyike hivyo mapema. Uzoefu unaonyesha kuwa, makosa mengi yanatokana na Mdadisi kushindwa kufuata zile skip patterns vizuri, na inakuwa ni hatari sana kwenye kazi ya ILFS kwa kuwa Mhojiwa ataendelea kuulizwa maswali ambayo hayamhusu na kupoteza ubora za Takwimu zetu.

Mwandiko uwe mzuri wa kusomeka ili wanaoingiza takwimu wasifanye makosa. Pia kama dodoso zaidi ya moja limetumika inabidi alama ya “X” ionyeshwe kwenye dodoso la kwanza na dodoso la…….kati ya …….pajazwe vizuri. Inabidi pia mdadisi kwenye dodoso la pili aanze na namba 13 kwa kuwa dodoso la kwanza lina uwezo wa kuorodhesha wanakaya 12. Ahakikishe kuwa, utambulisho umehamishiwa vizuri kwenye dodoso la pili kama ilivyokuwa kwenye dodoso la kwanza, kasha yabanwe vizuri na pini.

## MAENEO YANAYOHITAJI UKAGUZI NA UANGALIZI MAALUMU (SPECIFIC ISSUES)

## 2) SAMPULI YA KAYA ZILIZOCHAGULIWA

- ✓ Msimamzi anatakiwa kuhakikisha kuwa, kaya zilizochaguliwa kufanyiwa mahojiano zimo ndani ya mipaka ya EA husika. Endapo kaya itakuwa imehama na imehamia ndani ya mipaka ya EA, Kaya hiyo inatkiwa ifuatiliwe na ihojiwe.
- ✓ Endapo kaya iyakuwa imehamia eneo ambalo ni nje ya mipaka ya EA, basi Msimamizi anatakiwa mapatie mdadisi kaya ya akiba aendelee na mahojiano.
- ✓ Endapo kaya itakataa kuhojiwa, Msimamizi kwa kushirikiana na viongozi wa Mitaa na Vitongoji waweke bidii ya ziada kabisa kuelewesha kaya umuhimu wa takwimu hizi kwa

ujumla wake, usiri na namna takwimu hizi zitakavyotumika kwa manufaa ya Umma. Endapo itashindikana kabisa, kulingana na utafiti huu matokeo ya Utafiti kwenye kurasa wa juu wa dodoso pajazwe geresho namba 4 (Kaya imekataa kujibu) na hapatakiwi kchukua kaya ya akiba.

**3) UTAMBULISHO**

- ✓ Msimamizi anatakiwa kuhakikisha kuwa, utambulisho umejazwa vizuri kwenye dodoso kama ilivyo kwenye ramani za EA, pamoja na taarifa nyingine zilizoko kwenye ukurasa wa juu wa dodoso. Pia taarifa za Mdadisi na Msimamizi kwenye ukurasa wa pili ziwe zimejazwa kwa ukamilifu.

**4) LFS1 - TAARIFA ZA JUMLA ZA WANAKAYA**

- ✓ Hakikisha kuwa, kwa wanakaya wote walioorodheshwa kuna mkuu wa kaya mmoja tu kwenye swali la 3
- ✓ Umri wa Mkuu wa Kaya uwe reasonable....mfano Mkuu wa kay kuwa umri wa miaka 8
- ✓ Hakikisha kuwa, umri wa wanakaya ni sahihi kwa kuangalia mwezi na mwaka ulioandikwa kwenye swali 5A na 5B.
- ✓ Kama kwenye sw.3 kuna jibu lenye geresho 5 (Mazazi) hakikishwa tofauti ya umri wa Mkuu wa Kaya na Mazazi ni reasonable
- ✓ Pia kama kwenye sw.3 kuna jibu lenye geresho 3, hakikisha tofauti ya umri wa Mkuu wa kaya na mtoto ni reasonable
- ✓ Kama kuna geresho na 2 kwenye sw.3 hakikisha jinsi kwenye sw.4 ziko tofauti
- ✓ Wanakaya wote wenye umri chini ya miaka 5 waishie swali la 8
- ✓ Sw. 6: Anaulizwa mwanakaya mwenye miaka 45 au zaidi.
- ✓ Angalia hali ya ndoa kwenye swali la 9 kwa wenye miaka chini ya 12 kwa kujihakikishia kama wakiwa wameoa au kuolewa…yani kama wana geresho namba 1
- ✓ Linganisha majibu yaliyotoloewa kwenye Swali 11 na umri wa mwanakaya kwenye swali la 5B

**5) LFS1 - ELIMU NA MAFUNZO**

- ✓ Sw. 15:
    - ▪ Ikiwa jibu ni 1au 2 →Sw. 17A
    - ▪ Ikiwa jibu 3→Sw. 16 halafu nenda Sw. 17A

- Ikiwa jibu ni 4 → Sw. 16 halafu nenda Sw. 18

- ✓ Sw.17A, hakikisha kuwa waliopewa geresho namba 20 na 21 wanaulizwa sw.17B ili kuweza kupata aina ya fani waliyosomea, pia wenye geresho 00-18 wakaulizwe swal 18 pamoja na waliokuwa na geresho 20 na 21 kwa kuwa, inawezeka mtu akawa ana digrii ya Takwimu lakini pia amehudhuria mafunzo mengine ambayo yamemuongezea ujuzi kwenye kazi zake. Maswali haya ni muhimu sana kwa kuwa yatapima kiwango cha qualifications na skill match kwenye kazi anayofanya mhojiwa.

- ✓ Sw. 22B:
  - Linaulizwa iwapo jibu ni 1 katika Sw.22A(ii)
- ✓ Sw.20 linganisha mwaka wa kuhitimu mafunzo na umri wa mwanakaya kwenye sw.5B

- ✓ Maswali haya yameboreshwa zaidi kwa kuwa kutokana na Utafiti wa 2006, Uchambuzi uliofanywa na ILO, kiwango cha wafanyazi ambao walikuwa underqulification kilikwa zaidi ya asilimia 90. Kuna haja ya kuweka bidii kuhakikisha maswali haya yanajibiwa vizuri ili kupata takwimu bora zaidi.

## 6) LFS1 - UCHUMI WA KAYA KWA UJUMLA

- ✓ Maswali ya 22A hadi 25 yanalenga kupata hali ya uchumi wa kaya kwa ujumla wake, kuna haja sana ya kuhakikisha maswali yanajibiwa vizuri kwa kuwa yatatumika kama cross check kwenye maswali ya Kipato cha kaya kwenye maswali ya 61A – 63D.

- ✓ Kwa mfano, kama sw.22A linaonyesha kuna mwanakaya ana ajira ya mshahara, na swal la 61A likawa geresho 2 yaani hapana kwa wanakaya wote, inabidi mdadisi na wewe Msimamizi mrudi kwenye kaya kuhakikisha kama kulikuwa na makosa kwenye sw. la 22A. Maswali haya ni muhimu sana kuwa ni kigezo kimojawapo katika kupima Kazi zenye staha (descent work).

## 7) LFS2 - SHUGHULI ZA KAWAIDA

- ✓ Hakikisha waliojibu maswali haya ni wale wenye umri wa miaka mitano na kuendelea tu. Walio na geresho 1 kwenye sw.1 LFS2

- ✓ Maswali haya ni muhimu sana katika kupima shughuli za kawaida za mtu kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kwa kawaida ni vigumu mtu akawa hajafanya shughuli yoyote ya kiuchumi kwa kipindi cha miezi 12, hivyo hatutegemei kuona jibu la hapana isipokuwa kwa sababu maalumu kama mlevu asiyejiweza nk.

- ✓ **Kumbuka kuwa, Tanzania imeteuliwa kama nchi ya majaribio kwa Nchi za Afirica kupima maana ya ajira kwa kutumia tafsiri mpya**. Pamoja na maswali mengine, Sw.2 ni swali jipya kabisa kama lilivyopendekezwa na ILO ili kupima maana ya ajira kwa kutumia vigezo vilivyoboreshwa zaidi. Umakini mkubwa unatakiwa ili majibu yatakayotolewa yaweze kuonyesha picha halisi ya maana ya ajira kwa nchi zinazoendelea kama linakidhi haja.

- ✓ Sw.4 limeboreshwa kulingana na mapendekezo ya ILO na World Bank ili kupata viashiria vya kawaida vya hali ya ajira nchini. Swali hili linahitaji umakini sana wakati wa kumuuliza na kujaza kwa kila mwezi.


  Kama mtu atakuwa hakufanya kazi kwa kipindi chote cha miezi 12 iliyopita kwenye sw.3, basi mtu huyo atakuwa amefanya kazi kwa vipindi tofauti kwa miezi 12 iliyopita, kuna jedwali maalumu la kuweza kupata hali yake ya ajira kwa kila mwezi kwa kutumi jedwali la swal. 4A, na kujaza mageresho yafuatayo:-

  (i) alifanya kazi kwa mwezi mzima…A,
  (ii) Sehemu ya mwezi na alikuwa tayari kufanya kazi…B,
  (iii) Sehemu ya mwezi na hakuwa tayari kufanya kazi….C
  (iv) Hakufanya kazi kabisa na alikuwa tayari kufanya kazi….D
  (v) Hakufanya kazi kabisa na hakuwa tayari kufanya kazi…..E

- ✓ Msimamizi hakikisha mdadisi ameanza kwa kuweka alama "X" juu ya mwezi wa utafiti. Pia kajaza ndani ya visanduku kulia kwa alama "X" kwa kuanza na namba "1" na kuishia na namba "12". Kwa kuanza na mwezi kamili uliopita, “mwezi wenye namba 1", mhojiwa awe ameulizwa kwa kila mwezi kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita.

- ✓ Hakikisha kuwa, A + B + C + D + E = 12 kwa kila mwanakaya aliyejibu sw.4
- ✓ Taarifa hizo zitatuwezesha kukokotoa wale waliokuwa usually employed, usually unemployed na vishiria vinginevyo ya usuall employment

**MUHTASARI WA KUKAGUA SHUGHULI ZA KAWAIDA**



## 8) SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA SASA

- ✓ Wasimamizi inabidi mfahamu kwamba, kama ilivyosisitizwa wakati wa mafunzo, kulingana na vigezo vya Kimataifa, viashiria vyote vinavyotumika katika kupima na kutadhmini hali ya ajira nchini vinatokana na shughuli za kiuchumi za sasa (kipindi cha wiki moja iliyopita)

- ✓ **Kutokuwa kazini kwa Muda:** Hakikisha kwamba mtu ambaye hayuko kazini kwa muda anaorodheshwa kama anafanya kazi kwa kipindi ambacho hakuwa kazini. Hakikisha concept hii imeelweka vizuri kwa mdadisi na mhojiwa kwa kuwa ni mwongozo mkubwa sana wa kupata idadi kamili ya Nguvu Kazi ya Taifa. Kama haijaeleweka vizuri rudia kusoma mwongozo kama tulivyoelekezana kwenye mafunzo. Kumbuka mifano ifuatayo:-
    - o kazi za mishahara – likizo ya malipo, likizo bila malipo kwa muda usiozidi miezi mitatu bila malipo na baadaye kurudi kazini
    - o biashara/kilimo. –kutokuwepo kwenye biashara/kilimo kwa muda usiozidi mwezi mmoja wakati biashara/kilimo ikiendelea
    - o wafanyakazi wasiolipwa na vibarua hawahusishwi kwenye kundi la wasiokuwepo kazini kwa muda.

- ✓ Kumbuka **kuwa, Tanzania imeteuliwa kama nchi ya majaribio kwa Nchi za Afirica kupima tafsiri mpya ya ajira**. Pamoja na maswali mengine, Sw.22B ni swali jipya kabisa kama lilivyopendekezwa na ILO ili kupima maana ya ajira kwa kutumia vigezo vilivyoboreshwa zaidi. Umakini mkubwa unatakiwa ili majibu yatakayotolewa yaweze kuonyesha picha halisi ya maana ya ajira kwa nchi zinazoendelea kama linakidhi haja.

- ✓ Maswali haya yatatusaidia kupata viashiria vyote muhimu kama,
    - (i) Ukosefu wa ajira
    - (ii) Shughuli kuu
    - (iii) Sekta isiyo ras - sh_kuu
    - (iv) Shughuli nyingine ya kiuchumi
    - (v) Saa_zilizotumika
    - (vi) Mapato
    - (vii) Watoto


**9) SHUGHULI KUU NA SHUGHULI NYINGINE**

- ✓ Kumbuka kwamba, kama mtu hakufanya kazi yoyote sw.7 kwa wiki iliyopita na ana kazi ambayo anatajia ataendelea kuifanya kwenye sw.8A, basi hakikisha mtu huyo ameulizwa sababu za kutokufanya kazi sw.8B. Pia mtu huyo aulizwe kama hiyo kazi ilikuwa ni kazi yake kuu sw.8C.
- ✓ Kutokana na swali la 8C msimamizi hakikisha shughuli kuu imeandikwa vizuri kwa **angalao maneno mawili kwenye sw.18A** na **ENDAPO;** mhojiwa atasema kazi ambayo anatarajia kuendelea nayo siyo kazi yake kuu yaani awe na geresho 2 (hapana) kwenye sw.8C, basi hakikisha mdadisi ameandika **shughuli kuu kwenye Sw.18a** na shughuli ya **sasa kama shughuli nyingine kwenye Sw. 36a**

- ✓ Sw10. **Endapo** mhojiwa atatoa sababu za kutokuwa kazini wiki ilyopita kuwa ni geresho 2(Hana Mtaji) au geresho 4 (hana uwezo wa kuajiri msaidizi) inabidi mdadaisi arudi arekebishe sw. 9 kuwa alikuwa tayari kufanya kazi apewe geresho 1 na akaulizwe maswali ya ukosefu wa ajira kuanzia sw.11 hadi 17 C.

- ✓ Sw.14 Kama mhojiwa atakuwa ametoa sababu za kutokutafuta kazi kwa muda wa wiki nne (4) zilizopita kuwa ni ailikuwa **mgonjwa geresho 6** inabidi kurudi na kukagua Sw.8A na kumpatia geresho 2 kuwa hakuwa na kazi anayotarijia kuendelea nayo. **PIA kama sababu aliyotoa ni Mwanafunzi muda wote (geresho la 7)** inabidi kurudi na kukagua Sw. **kukagua Sw.9 na kumpatia geresho 2 kuwa hakuwa tayari kufanya kazi**

## MUHTASARI WA KUKAGUA UKOSEFU WA KAZI NA KUTOKUWA TAYARI KUFANYA KAZI



## 10) SAA ZA KAZI/SHUGHULI ZA KIUCHUMI WIKI ILIYOPITA

- ✓ Sw.53A, Hakikisha kila mhojiwa amejaziwa saa alizofanya kazi kwa kila siku kuanzia Jumatatu hadi Jumapili. Swali hili ni muhimu sana katika kupima kiwango cha ajira isiyo timilifu kwa kutumia kigezo cha masaa.

- ✓ Sw. 53A: Jibu ni 00 iwapo Sw.7 = 2 na Sw.8A=1

## 11) SEKTA ISIYO RASMI

Hakikisha sw. 31 na sw. 49 kwa kulinganisha na muda wa biashara/shughuli

## 12) MAPATO YATOKANAYO NA KAZI/SHUGHULI ZA KIUCHUMI

- ✓ Sw. 61A: Jibu ni 1 iwapo Sw. 20/38 = 1
- ✓ Sw. 62A: Jibu ni 1 iwapo Sw. 20/38 = 2 au 3
- ✓ Sw. 63A: Jibu ni 1 iwapo Sw. 20/38 = 8 au 9 au 10
- ✓ Hakikisha kuwa kiasi cha mapato/fedha yaliyobakia/ zilizobakia kwenye biashara/shughuli baada ya kutoa gharama zote katika kipindi cha wiki/mwezi uliopita itakuwa ni swa na (sw.62b–sw.62c)

## 13) DODOSO LA WCS

- ✓ Dodoso hili la WCS linakusanya taarifa za kila mtoto mwenye umri kati ya miaka 5 - 17 kwenye kaya iliyochaguliwa. Taarifa zitapatikana kwa kumhoji mtoto mwenyewe kwenye kaya husika na ikiwa mtoto atashindwa kujieleza mwenyewe, mzazi au mlezi anaweza kumsaidia kutoa taarifa atakazoshindwa kuzitoa.

- ✓ Hakikisha umri wa mtoto kwenye sw.5B LFS1 kama ana umri kati ya miaka 5 hadi 17

- ✓ Dodoso hili linakusanya taarifa za hali ya ajira kwa watoto. Mtoto aulizwe taarifa juu ya shughuli/kazi za kiuchumi au zisizokuwa za kiuchumi alizozifanya. Taarifa zinazopatikana ni muhimu sana kwa ajili ya kujua ni kwa kiasi gani mtoto amejihusisha kwenye kazi za kawaida na shughuli za sasa kupitia saa zilizotumika kwa kazi, mapato, masuala yahusuyo afya na usalama kazini.

- ✓ Ikiwa mtoto hawezi kujieleza mwenyewe, msimazi hakikisha mdadisi anajaza namba ya mwanakaya aliyemjibia kwenye sehemu husika ILFS2 ukurasa wa 1. Hii itasaidia kuchambua uhakika wa majibu kati ya watoto wanajibu wenyewe na wale wanaojibiwa.

- ✓ Msimamizi hakikisha taarifa za mtoto ziko sahihi katika mstari wa namba aliyopewa kwenye orodha ya wanakaya kutoka kwenye dodoso la LFS1 sw.1, mfano: ikiwa mtoto yupo namba 09, hakikisha taarifa zake zimeandikwa katika mtari namba 09 hata kama mistari ya juu ipo wazi.

**14) SHUGHULI ZA KAWAIDA ZISIZO ZA KIUCHUMI KWA WATOTO WA MIAKA 5 – 17 KWA KIPINDI CHA WIKI ILIYOPITA. (MDADISI: ULIZA KWA WATOTO WOTE)**

- ✓ Msimamizi hakikisha swali la 1 katika sehemu hii linaulizwa kwa watoto wote wenye umri wa miaka 5-17, katika kaya za kawaida mara nyingi watoto hushiriki shughuli ndogondogo za kaya kama kununua bidha kwa ajili ya kaya, usafi wa nyumba, kuosha vyombo, nk. Hakikisha mdadisi anatoa ufafanuzi juu ya aina za shughuli za nyumbani sw.1.

- ✓ Kisha ajaze saa zilizotumika katika kufanya shughuli za nyumbani sw.2, Msimamizi hakikisha mdadisi anajaza saa zilizotumika kwa shughuli hizi tu na asichanganye na shughuli za kiuchumi, Hakikisha mdadisi ametoa maelekezo ya kutosha kwa mtoto ili asichanganye na saa za kazi za kiuchumi.

**15) MAHUDHURIO SHULENI NA SAA ZA KAZI**

- ✓ Sehemu hii inakusudia kupata taarifa za madhara wanayopata watoto kielimu kutokana na kujishughulisha na kazi, ni muhimu kuhakikisha kuwa sw. 3A linajibiwa kwa umakini likihusisha majibu aliyoyatoa mtoto kwenye LFS 2 Sw. 1, au Sw. 7, au Sw. 8A au WCS Sw. 1.

- ✓ **Msimamizi: Swali la 4** linataka kujua iwapo kufanya kazi kwake kunaathiri mahudhurio au masomo yake, msimamizi hakikisha mdadisi anamwelewesha vizuri mtoto aelewe vizuri swali hili. Mtoto aelekezwe kuwa swali linalenga kujua madhara anayoyapata kielimu tu na siyo vinginevyo.

## 16) WATOTO WALIOFANYA SHUGHULI ZA KIUCHUMI WIKI ILIYOPITA

- ✓ Sehemu hii wajibu watoto waliloonesha kuwa wamefanya shughuli za kiuchumi kwenye dodoso la LFS2, uzoefu unaonesha kuwa maswali yanayohitaji mdadisi kurejea nyuma ili kajua kama aendelee na maswali au la, huwa na matatizo sana. Mara nyingi wadadisi hukosea na kuhoji maswali yasiyowahusu. Hivyo msimamizi hakikisha unakagua vizuri kama waliojibu maswali ya sehemu hii ni wale tu wanaostahili, ni rahisi kubadili majibu yaliyokosewa ukiwa field kwa kurudi kwenye kaya na kuhakiki majibu.
- ✓ Watoto wanaotakiwa kujibu swali hili ni wale waliojibu sw.18A au 36A kwenye LFS2

## 17) AFYA NA USALAMA WA WATOTO WALIOFANYA KAZI ZA NYUMBANI AU ZA KIUCHUMI MIEZI 12 ILIYOPITA AU WIKI ILIYOPITA

- ✓ Maswali katika sehemu hii yanalenga kupata taarifa za madhara ya kiafya yanayotokana na shughuli za aina yoyote, madhara haya yawe yametokea wakati wa kufanya shughuli hiyo au katika maeneo hayo.

## 18) MAONI YA MTOTO KULINGANA NA KAZI/SHUGHULI ANAZOFANYA

- ✓ Msimamizi hakikisha kuwa mdadisi anawahoji watoto wenye umri wa miaka 5-17 ambao walifanya kazi/shughuli za kiuchumi katika kipindi cha wiki iliyopita yaani waliojibu Sw. 18(A) au Sw. 36(A) kwenye dodoso la LFS 2. Kwa wale watakaooneka wamejibu swali hili, kagua maswali yaliyoainishwa hapo juu kama yamezingatiwa.

## 19) DODOSO LA UTAFITI WA MATUMIZI YA MUDA

- ✓ Hili dodoso linatarajia kukusanya taarifa za mwanakaya mmoja tu kwa kila kaya mwenye umri wa miaka 5 au zaidi.
- ✓ **Msimamizi hakikisha utaratibu wa kumchagua mwanakaya anayestahili kuhojiwa TUS umefuatwa kwa kutumia KISH GRID procedure kama ilivyoelekezwa kwenye mafunzo.**
- ✓ Hakikisha Jinan a Namba ya mwanakaya aliyechaguliwa inaandikwa kwenye ukurasa wa kwanza wa Dodoso la TUS kwenye maeneo yaliyoainishwa

- ✓ Msimamizi hakikisha mdadisi anamweleza mhojiwa kwamba utafiti huu unahitaji kujua ni jinsi gani Mwanakaya alitumia muda wake katika kufanya shughuli zote za kiuchumi na zisizo za kiuchumi kwa saa 24 kwa siku katika siku iliyopita.

- ✓ Msimamizi hakikisha mdadisi anauliza maswali yote, kama kuna shughuli alizifanya kwa wakati mmoja zote zionyeshwe kwenye orodha ya shughuli kama ilivyoanishwa kwenye dodoso.

- ✓ Msimamizi hakikisha mdadisi anauliza maswali yote kuanzia swali la 1 hadi swali la 13, uzoefu unaonesha kuwa wadadisi hujisahau na kuishia swali la 5b, hivyo ni bora kuhakikisha maswali haya yanajibiwa kiukamilifu ukiwa field.

- ✓ Hakikisha mdadisi anajaza matukio yote muhimu ya mhojiwa, matukio haya yanajumuisha kulala, kula, kusafiri (kutoka kwenye kaya kuelekea sehemu nyingine), kupumzika, usafi wa mwili. Kila mwanakaya huhitaji matukio haya ili aishi, hivyo inategemewa kwa sehemu kubwa kila mwanakaya atakuwa na matukio haya, usipoyaona, nenda kahoji kujihakikishia kama kweli hayakutokea.

- ✓ Msimamizi hakikisha mdadisi anajaza angalau tukio moja katika kila saa kwenye saa zilizoainishwa kwenye dodoso. Haitegemewi kukuta saa haina tukio, kwa kuwa kama mwadamu yupo hai basi lazima atakuwa na tukio katika kila saa ya siku (mfano kupumzika, kulala, nk).

- ✓ Msimamizi hakikisha mdadisi anatenganisha matukio ya kusafiri kuelekea kwenye shughuli za uzalishaji wa awali kama shambani na kazi za ajira au viwandani, hii itasaidia kutenganisha muda unaotumika kusafiri kuelekea kwenye shughuli hizi.

- ✓ Kwa matukio yanayoweza kufanyika kwa pamoja, msimamizi hakikisha mdadisi anaainisha matukio haya na kagua uhalisia wa matukio haya, mfano kulala hakuwezi kuendana na kuangalia runinga, ila kupumzika huenda kukafanyika pamoja na kuangalia runinga.

- ✓ Msimamizi hakikisha mageresho ya aina ya usafiri yajazwe kwa usahihi, hakikisha shughuli zinazofanyika ndani ya kaya hazihusishi usafiri.

**TAKWIMU BORA KWA MAENDELEO**